nce

Tanzania, cotton is among the strategic crops grown in 17 re-

250,000 tonnes to one million tonnes by 2025/2026 adding

zania Cotton Board (TCB), the Brazilian Cooperation Agency

intercropping systems for cotton with a view to improving the

project, his organization would provide technical project imple-

is why WFP decided to join into this crucial project."



***LIVESTOCK sector stakeholders attend a meeting that was addressed by Livestock and Fisheries Minister, Mr Mashimba Ndaki in Dodoma, yesterday. (Photo by Iddy Mwema)***

CamScanner

THE GUARDIAN Page 5.

# Livestock sector stakeholders embark on masterplan review before transformation

By Polycarp Machira, Dodoma

STAKEHOLDERS in the livestock sector have embarked on review of the Livestock Master Plan ahead of launch of the new five-year livestock master plan.

The new strategy, 'Livestock Sector Transformation Plan (LSTP)' will build on the successes of earlier plan to strengthen breeding and animal health programmes.

LSPT provides sector actors with evidence on where to invest in the livestock sector to achieve national development goals as well as meet Tanzania's regional and global committees such as Comprehensive African Agriculture Development Programme (CAADP) and Sustainable Development Goals (SDGs).

The original plans was launched in 2017 as a collaborative development plan between the government, the private sector and non-governmental organisations to identify and strengthen priority livestock value chains and production systems.

Its goal was to translate the national livestock sector's priorities into realistic and achievable time-bound targets and objectives while guiding the sector's investment decisions.

Speaking while officiating the opening of a meeting that brought together development partners, the private sector, civil society and the media, Minister for Livestock and Fisheries, Mashimba Ndaki called on the participants to critically discuss what to improve in the 2022/23-2026/27 plan.

While stressing on the importance of the livestock to the nation, he acknowledge the key roles played by development partners and the private sector in developing the sector and improving livelihood of Tanzanians.

He said the government is playing regulation roles in a sector dominated by private player. According to the minister, the government has only about 100,000 animals in its ranches while the remaining of the 35 million livestock belongs to private sector.

The minister said while several gains have been realized in the livestock sector, a lot more need to be done to increase the sectors contribution to the national economy and improvement of individual livelihoods.

"The sector can help create jobs, bring foreign currency and strengthen national development." he said, adding that such stakeholders meetings can help identify what needs to be done to improve investment in the sector.

Acting Permanent Secretary in the ministry, Dr Charles Mhina on his part noted that the meeting was to discuss successes and challenges realized in the implementation of the previous plan. "In the past five years we have realised the strength of the sector in creating development changes and we now need a common understanding implementation of the new plan," he said.


Jane Goodall Institute
TANZANIA
For Wildlife Research, Education & Conservation

JOB OPPORTUNITY

**About Us:**
The Jane Goodall Institute (JGI) is a global community conservation organization that advances the vision and work of Dr. Jane Goodall by conserving chimpanzees and inspiring communities to conserve the natural world we all share, we improve the lives of people, animals, and the environment, we strongly believe everything is connected and everyone can make a difference. The Jane Goodall Institute (JGI) was founded in 1977 by Dr. Jane Goodall (DBE).

JGI Tanzania is currently seeking to recruit suitably qualified and competent candidate to fill the following vacant position:

*Job Vacancy:* **Roots & Shoots Community Coordinator**
**Workstation:** In one of JGI's Africa offices
**Reporting Line:** Vice President for JGI Africa Programs

**Application Procedure:**
To apply for this position, please go to: https://www.janegoodall.org/about/jobs/

Only the shortlisted candidates will be contacted for the interview.

**Deadline:** Seven (7) days from the date of the first appearance of this advertisement on the newspapers.

**JGI Tanzania is an equal opportunity employer and considers all applicants on the basis of merit without regard to race, national or tribal origin, religious belief, sexual orientation, and marital status.**

QUALIFIED WOMEN ARE HIGHLY ENCOURAGED TO APPLY.

216954501


CamScanner

umma. katika maeneo ya miji na kuhakiki- Aliitaka bodi itambue viwanja Alisema pamoja na kujen

HABARI LEO UK 8.



Naibu Waziri wa Mifugo, Abdallah Ulega (kulia) akimsikiliza Ofisa Mauzo wa Agricom Africa Kanda ya Mashariki, Mkali Crispo akitoa maelezo kuhusu matumizi ya zana za kampuni hiyo kwenye maonesho ya kwanza ya wafugaji wanaofuga kibiashara yaliyofanyika Ubena Zomozi, Halmashauri ya Chalinze, Mkoa wa Pwani juzi. (Picha na Wizara ya Mifugo).

## ...Wataalamu wataja mbinu kuukabili mgunda nyumbani

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAMU wa magonjwa na mifugo nchini wametoa mbinu mbalimbali za kujikinga na ugonjwa wa mgunda majumbani baada ya kuthibitisha kuwapo kwa watu wanaougua ugonjwa huo nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alisema jana kuwa ili kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa huo jamii ihakikishe nyama wanazokula, zimepimwa na wataalamu na kuthibitishwa usalama wake na kuwa makini na nyama za porini, hasa panya.

"Tunawashauri watu kwamba waache kula vitu visivyoliwa kikawaida, wale panya ndiyo chanzo cha shida na kule Mtwara na Lindi wanawala sana wale panya," Prof. Hezron alionya.

Kuhusu mifugo, Prof. Hezron alisisitiza jamii ihakikishe inawapatia chanjo na kupunguza mwingiliano wa wanyama wa kufugwa na wa porini ili kuepusha maambukizi kwa kuwa binadamu wapo karibu na wanyama hao.

"Kwa maana hiyo ni kwamba kwa sababu mbwa anafugwa katika mazingira ya nyumbani, watu wachukue tahadhari ya kudhibiti panya, kwa sababu ndiyo chanzo kikuu cha ugonjwa huu kuja kwenye mazingira ya nyumbani.

"Hawa ndio wanautoa kwa wanyama wa porini huko kama simba, nyati na kuuleta huku," alifafanua.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa ipo mifugo na wanyama wengi wa porini ambao wana maambukizi lakini hawaugui huku wanyama kama ng'ombe, kiwango cha maambukizi kikiwa ni asilimia 5.5 mpaka 50 kulingana na eneo.

Mkurugenzi wa Kuratibu na Kukuza Utafiti wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Dk. Paul Kazyoba, akizungumza na RadioOne jana, aliishauri jamii isipende kwenda kulisha mifugo kwenye mazingira yenye wanyamapori kwa kuwa huko ndiko wanaambukizwa magonjwa hayo.

Pia alishauri mifugo ichinjwe kwenye maeneo rasmi ili nyama yake ikaguliwe na wataalamu wa afya kama ni salama kwa matumizi ya binadamu, pia kula nyama iliyoiva vizuri na maziwa au maji yaliyochemshwa vyema.

Mkurugenzi huyo aliitaka jamii kuzingatia usafi wa mazingira ya nyumbani ili kudhibiti wanyama hasa panya ambao kuingia kwao ndani kunawaachia bakteria wanaosababisha ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa NIMR, Sayoki Mfinanga, aliishauri jamii inayofuga, ihakikishe inapeleka mifugo hiyo kwa wataalamu wake pale wanapoona wanaugua ili kufanyiwa vipimo, kupatiwa dawa na ushauri.

Mwanzoni mwa wiki, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema ugonjwa huo ni miongoni mwa magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na unasababishwa na bakteria aina ya leptospira interrogans.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjian, kabla ya mazungumzo yao, ofisini kwake, Ikulu Magogoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# Tahadhari yatolewa walaji nyama choma homa mgunda

**Na Martha Magawa**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imewataka wananchi kuchukua tahadhari wanapohitaji kula nyama choma kwa kuhakikisha chanzo chake ni salama na inaiva vizuri ili kuepukana madhara kwa walaji.

Rai hiyo ilitolewa na Dk. Azma Simba, kutoka wizara hiyo ambaye ni mtaalamu wa afya ya jamii katika fani ya epidemiolojia wakati akizungumza na Nipashe kupitia mahojiano.

Azma alisema kuwa ulaji wa nyama ambayo haijaiva vizuri ni hatari kwa afya ya walaji na kuwataka wananchi wachukue tahadhari wakati tayari serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa mikoa ya Kusini mwa Tanzania kulikotangazwa mlipuko wa ugonjwa wa Mgunda na kuripotiwa watu 20 kugundulika kuwa nao na watatu kati yao kupoteza maisha.

"Kwa wale watumiaji wa mishikaki au nyama choma yoyote wahakikishe kuwa vyanzo vyao ni salama na nyama ile inakuwa imekaguliwa ili kuepusha madhara ya kiafya ikiwamo homa ya Mgunda na magonjwa yoyote yanayoambukizwa na wanyama," alisema Azma.

Pia, alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wizara nyingine ikiwamo Maji, wataalamu wa mazingira na wanyama pori, wafanyakazi kwa pamoja chini ya mpango wa Afya Moja 'One Health' utasaidia kuondoa au kumaliza adha wanazokutana nazo wafugaji ikiwamo ukosefu wa majisafi na salama kwa jamii za wafugaji.

"Milipuko ya magonjwa yatokanayo na mifugo chanzo kikubwa ni kukosekana kwa huduma za majisafi na salama kwani wafugaji wanatumia maji pamoja na wanyama na mara nyingi bila kuchemsha maji hayo," alisisitiza Azma.

Wakati huo huo, Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dk. Shadrack Mwaibambe, alisema ongezeko la wafugaji katika mikoa ya Kusini limetokana na wafugaji wengi kuhamia kutoka mikoa ya Kanda ya Kati na vyanzo vya maji kuzidiwa.

Kuhusu masuala yanayohusu afya, alisema wamekuwa wakiachiwa mzigo kubwa wataalamu wa afya jambo ambalo amelitaja kuwa sio sahihi na kushauri wanasiasa kuongeza nguvu kwa kuzungumza na wananchi wao ili kwa pamoja elimu iwafikie kwa wingi ili kuepusha athari zinazotokana na magonjwa ya milipuko.

# IGP Wambura aanza na wahalifu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura, ametangaza vita dhidi ya wahalifu, akionya kuwa kamwe wasifikiri ni ajira kwa kuwa jeshi litatumia nguvu kubwa na za kisasa kuhakikisha wananchi wanakuwa salama na serikali inaendelea na shughuli zake.

IGP Wambura alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti juzi baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo na jana asubuhi alipoanza kazi rasmi na kuonekana akiwa jijini Arusha kwa ajili ya Mkutano wa 22 wa Wakuu wa Nchi saba za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Juzi baada ya kuapishwa, aliripoti Makao Makuu ya Polisi jijini Dodoma na kukabidhiwa rasmi ofisi na mtangulizi wake, Simon Sirro, ambaye ameteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania huko Zimbabwe.

Akizungumzia mikakati yake ndani ya Jeshi la Polisi, IGP Wambura aliitaja mitatu, ukiwamo wa kukabiliana na uhalifu nchini.

"Mikakati yangu mikubwa ambayo nitatekeleza kwa kushirikiana na makamishna walio chini yangu pamoja na kada mbalimbali za askari na viongozi waliopo ndani ya Jeshi la Polisi, kwanza ni kuhakikisha suala la uhalifu mapambano dhidi ya uhalifu yanaimarishwa.

"Wahalifu wasije wakafiriki kwamba ile ni ajira, hakuna hiyo na nguvu ambayo tutatumia kupambana na uhalifu ni kubwa lakini nguvu ya kisasa.

"Na tutahakikisha wananchi wanakuwa salama na serikali inaendelea na shughuli zake na kutokuwa na fikra za kuona ni namna gani wataanza tena kushughulika na uhalifu na kuweka rasilimali zao pale. Kazi yangu kubwa ni kuhakikisha suala la uhalifu linakoma," alionya.

IGP Wambura alitaja jambo la pili ni kushughulika na maadili ndani ya Jeshi la Polisi, akisisitiza hawawezi kuwa na jeshi zuri, imara la kisasa na lenye weledi kama hakuna maadili na nidhamu.

Alitaja suala la tatu ni haki kwa wananchi, akifafanua kuwa linajumuisha kuwa na vituo vya polisi vingi na kuhakikisha kuna askari wanaofanya kazi.

"Tunataka kuona watu wanatendewa haki kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu. Hii ni baadhi ya mikakati ambayo nitahakikisha inafanyiwa utekelezaji, inakuwa inasimamiwa na yote itaweza kuleta tija katika Jeshi la Polisi," alisema.

Akiwa jijini Arusha jana, IGP Wambura alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha wakati wote wa mkutano huo, kunakuwa na ulinzi madhubuti kwenye maeneo yote.

Juzi, Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kumwapisha IGP Wambura, alisema anachotegemea kutoka kwake ni mabadiliko makubwa ndani ya Jeshi la Polisi ili kuwe na ufanisi ndani ya jeshi hilo, pia usalama wa raia na mali zao uimarishwe.

CamScanner

# Umuhimu wa misitu katika kilimo na mifugo

Na Dk. Felician Kilahama

HAKUNA aliye kama Bwana Mungu wetu anayeishi milele yote: Alpha na Omega tumshukuru kila wakati na kila mwenye pumzi amsifu yeye aliyetuumba kwa sura na mfano wake. Katika makala iliyopita nilieleza umuhimu wa miti/misitu kwa kujikita zaidi katika miti ya kupanda (masamba ya miti), matumizi na faida zake.

Kupitia makala haya, hebu kwa pamoja, tuchunguze kwa undani zaidi misitu ya asili na ukaribu wake na sekta za kilimo na mifugo. Tangu tupate uhuru Desemba 9, 1961 mpaka sasa sekta za kilimo na mifugo zimekuwa ni maeneo muhimu katika Sera na miongozo ya Taifa kwa ujumla.

Kilimo huwa kinafahamika kama 'uti wa mgongo' kwa taifa. Ukiongeza na mifugo umuhimu wake unapanuka zaidi maana ni haohao wakulima pia niwafugaji. Miaka ya mwanzoni tangu kupata uhuru walikuwepo wafugaji ambao walijikita kwenye kufuga tu bila kulima; kama Wamasai au Wamang'ati. Wakati huo kukawepo Watanzania wasiojihusisha na kilimo wala kufuga. Mathalani, Wahadzabe wanaoishi maeneo ya mikoa ya Singida na Manyara. Watu hawa wamekuwa wakitegemea misitu kwa maisha yao ya kila siku kwa asilimia miamoja. Kwa ujumla ni kwamba misitu ni hazina kubwa kwa maisha ya binadamu.

Kwa nyakati tulizomo hali imebadirika waliokuwa wafugaji tu bila kulima sasa wameanza kulima. Wahadzabe nao siyo tena wa msituni wameanza maisha tofauti na hali yao ya zamani. Siku za usoni nitaweza kufafanua kwa nini ninasema hivyo kuhusu Wahadzabe.

Kwa utangulizi huo sasa tuangalie kwa undani uhusiano na madhara ya kilimo/ufugani kwa misitu. Watanzania wengi wanategema sana shughuli za kilimo na ufugaji ili kupata riziki za kila siku. Hata wafanyabiashara na wafanyakazi katika sekta mbalimbali za umma na binafsi, wananufaika na mazao ya kilimo na mifugo pamoja na misitu.

Hata hivyo, tangu uhuru takribani miaka 60 iliyopita shughuli za kilimo na ufugaji zimekuwa zikifanyika kwa kutumia teknolojia isiyo rafiki kwa rasilimali misitu na nyuki. Ingawa Watanzania zaidi ya asilimia sabini; wamekuwa wakitegemea kilimo na ufujaji kwa chakula na kipato.

Mbinu za kulima na kufuga, kwa miaka mingi, zilibaki kuwa ni kufyeka misitu na kupanda mazao na/au kuchunga mifugo. Maeneo mengi ya misitu ya asili yamekuwa yakifyekwa kwa ajili ya kupanda mazao na sehemu nyingine kuchungia mifugo.

Wakulima hufyeka na kulima eneo moja kama eka mbili au tatu kwa miaka miwili au mitatu halafu kuahamia sehemu nyingine. Kilimo cha aina hiyo kimeathiri sana misitu maana maeneo mengi yamekuwa yakifyekwa kwa madhumuni hayo. Takwimu za mwaka 2015 zinaonyesha Tanzania Bara imekuwa ikipoteza hekta 372,000 kila mwaka kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwepo kilimo na ufugaji; bila kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali misitu.

Kiwango hicho cha kutoweka misitu ya asili kimeongezeka katika mikoa ya Katavi, Kigoma, Rukwa na Tabora hadi kufikia takribani hekta 470,000 kwa mwaka kutokana na kasi ya kukata miti kuongezeka sana. Kilimo, mifugo, utengenezaji mkaa na makazi mapya vimechangia sana katika mikoa hiyo. Usimamizi wa misitu vijijini ni duni hivyo, watu wanafanya wapendavyo, lakini hasara ni kwa taifa zima.

Misitu na kilimo/mifugo vinashabikiana kwa maana kwamba misitu ni sehemu muhimu ya upatikanaji wa chakula na lishe kwa mifugo. Wakulima wengi nchini, kwa kuzingatia ujuzi wa kijadi, wanafahamu kuwa eneo lenye misitu au uoto wa asili wa kutosha, linarutuba nyingi na huhifadhi unyevunyevu ardhini hivyo, kuona misitu kama maeneo yanayofaa kwa kilimo. Kuna aina mbalimbali za miti kama Migunga zinazofaa kurutubisha udongo kwa kupitia mizizi yake.



*Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Nyasa mkoani Ruvuma, Bugingo Bugingo akimsikiliza Mratibu wa Mradi wa Forvac Mkoa wa Ruvuma, Marcel Mtunda alipotembelea mradi wa panda miti kibiashara katika kijiji cha Mkali A.*

Mjani hufyonza gesi aina ya oksijeni na nitrojeni na kupitia mizizi yake kuweza kutengeneza mbolea yenye nitrojeni ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa mzao. Wafugaji nao yanajua palipo na misitu hali ya majani inakuwa nzuri. Vilevile, wafugaji nao wanafahamu vema kuwa ndani ya misitu kuna lishe ya kutosheleza mahitaji ya wanyama wao na hasa nyakati za ukame mifugo huponea kwenye misitu na maeneo ya hifadhi hasa Mbuga za Wanyamapori. Aina za miti kama Migunga, Mibuyu, Albizia spp ni chakula cha wanyama.

Kwa wafugaji misitu ni sehemu muhimu ya kupata dawa asilia kutibu mifugo pindi inapoumwa hivyo kuboresha afya zao. Katika misitu kuna aina mbalimbali za mitishamba inayofaa kutibu wanyama na binadamu. Maeneo mengi ambayo yalikuwa yakilimwa na hatimaye kuachwa wazi yamepoteza rutuba kwa kiasi kikubwa kutokana na mmomonyoko wa udongo ambao husombwa na maji ya mvua na kuishia mabondeni au kujaza vina vya mito kama tunavyoshuhudia kwenye Mto Msimbazi, jijini Dar Es Salaam. Kwa upande mwingine upepo mkali pia hupeperusha chembechembe za udongo na kuzipeleka mbali hivyo kupunguza thamani ya eneo la kilimo.

Uharibifu wa misitu pia unatokana na uchomaji moto mapori na mbuga nyakati za kiangazi, lakini pia utengenezaji mkaa kiholela na kwa teknolojia duni. Hii husababisha pia maeneo yanayofaa kilimo kupoteza ubora wake haraka na kusababisha wakulima kuendelea kufyeka misitu hovyo.

Hatari nyingine ni kupungua maji na ardhi kuwa kame kiasi cha kuathiri mazao kwa kiwango kikubwa. Tukiunganisha na mabadiriko ya tabianchi kama tunavyoshuhudia siku hizi unyeshaji wa mvua nje ya msimu wake, upepo mkali na maeneo kama ya Pwani yenye historia ya joto kuwa na ongezeko la baridi siyo hali ya kawaida. Sehemu kama Mkoa wa Njombe baridi ni kali sana kiasi cha kusababisha hata barafu kutokea.

Kinachotakiwa sasa ni kuhakikisha misitu ya asili inarejea na kusimamiwa ipasavyo. Watu wasikate miti hovyo kana kwamba haina mwenyewe na badala yake tupande miti kwa wingi katika maeneo tunapoishi. Kila Mtanzania akipanda mti mmoja na kuutunza na wazazi wakawapandia watoto wao ambao bado wachanga tutakuwa na miti zaidi ya milioni 60 sawa na hekta karibu 40,000 mpaka 50,000 ya shamba la miti kulingana na nafasi kati ya mti na mti.

Pia napongeza hatua ya Serikali kuongeza bajeti kwa sekta ya kilimo na umwagiliaji kwa mwaka 2022/2023 zaidi ya Sh. bilioni 750 ukilinganisha na bilioni 294 kwa mwaka 2021/2022. Huu ni utashi mkubwa sana wa kisiasa kusababisha ongezeko la takribani asilimia 155. Kama fedha hizo zitatumika ipasavyo na watalaamu husika wakatimiza wajibu wao, naamani kwa miaka michache ijayo misitu ya asili inaweza kuimarika kwa kustawi vizuri na afya yake kuwa bora zaidi.

Kipekee nguvu iwekwe kwa maosifa ugani vijijini ili kwa pamoja na wakishirikiana vizuri wakawaelimisha wakulima na wafugaji namna ya kuendesha kilimo/ufugaji kijani; hatimaye wanufaika wataweza kutumia eneo dogo na kupata mazao mengi kwa ekari moja.